JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1575,
Simu: (026) 2700157
Nukushi: (026) 2703014
Baruapepe: rbciringa@pccb.go.tz
Mtandao : www.pccb.go.tz

IRINGA 10 JULAI, 2020

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU IRINGA YAFUNGUA MASHAURI MAPYA KUMI NA SITA MAHAKAMANI KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI, 2020

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Iringa katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020, imefanikiwa kufungua mashauri ya rushwa na makosa mengine kumi na sita (16) mahakamani.

Mashauri kumi na tatu (13) yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa na mashauri matatu (3) yalifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kilolo. Mashauri hayo kumi na sita (16) yanaendelea mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yote ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa kufikia therathini na tatu (33). Aidha, katika kipindi tajwa kesi moja (01) ilitolewa hukumu na mshtakiwa alipatikakana na hatia .

Ndugu wanahabari,

Vilevile Taasisi ya Kuzuia na Kupamnana na Rushwa Mkoa wa Iringa katika kipindi tajwa imeweza kufanya kazi mbalimbali za udhibiti na kufanikiwa kudhibiti na kuokoa mali na fedha kutokana na operesheni mbalimbali :-

Katika operesheni inayoendelea ya ufuatiliaji wa madeni ya wadaiwa sugu na chunguzi za ubadhirifu wa fedha za Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) hadi kufikia leo tarehe 10.07.2020 tumefanikiwa kuokoa jumla ya shilingi **1, 201,857,835/=** na tunaendelea na uchunguzi wa tuhuma za madeni hayo yenye jumla ya shilingi **3,706,111,828/=.**

Tulifanikiwa kurejeha mali kutokana na mikopo umiza ikiwa ni gari aina ya **NISSAN SERENA lenye Namba za usajiri T311 DDF** iliyokuwa mali ya mwalimu mstaafu HADIJA NASSOR MAZOLA aliyekopa kiasai cha shilingi 2,000,000/= mwaka 2017, kutoka kwa mkopeshaji wa mikopo umiza Bw. MICHAEL WILSON SANGA.

Katika kipindi cha mwaka 2017 aliweza kurejesha kiasi cha shilingi 4,000,000/= na mara baada ya kurejesha fedha hizo, mkopeshaji huyo alimweleza kuwa deni lake limefikia shilingi 12,000,000/=. Hivyo alimtaka kulipa shilingi 8,000,000/= zilizobaki na baada ya kushindwa kulipa ndipo alichukua gari hilo na kujimilikisha tangu mwaka 2017 hadi TAKUKURU Mkoani Iringa tulipoikamata.

Pia tulifanikiwa kurejesha **mashine ya kuchanganya zege (**concrete mixer) yenye thamani ya shilingi **6,321,000/=** mali ya Bw. Mtalemwa John Kaiza mmiliki wa Kampuni ya Lekansingo Construction Company Ltd kutoka kwa Bw. Abel Muyinga ambaye ni mkopeshaji wa mikopo umziza baada ya Bw. Mtalemwa John Kaiza kukopa shilingi 2,000,000/=kutoka kwa mkopeshaji huyo tarehe 30/10/2018. Baada ya kukopa fedha hizo alitakiwa amkabidhi mashine hiyo na ilipofika tarehe 12/02/2019 alikuwa tayari amerejesha shilingi 2,250,000/= ndipo mkopeshaji huyo alipomueleza kuwa deni lake limefikia shilingi 7,000,000/=ambapo mhusika alishindwa kulipa fedha hiyo.

Aidha, mkopeshaji aliendelea kushikilia mashine hiyo kwa kuifanyia biashara ya kuikodisha kwa wakandarasi mbalimbali kwa gharama ya shilingi 100,000/= kwa saa na fedha aliyopata aliitumia kwa msalahi yake binafsi hadi mashine hiyo ilipokamatwa na TAKUKURU Mkoani Iringa.

Tuliweza kufanya kazi ya udhibiti wa shilingi **20,572,434 /=** za uharibifu wa misitu iliyoko katika mlima wa Idelemle uliopo katika kijiji cha Makifu kata ya Mahuninga Wilaya ya Iringa ambapo miti 84 aina ya muheni ilivunwa kinyume na taratibu za uvunaji endelevu wa mazao ya misitu kama Mwongozo wa Uvunaji wa Misitu wa mwaka 2004, Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002, Kanuni za misitu za mwaka 1968 na Tangazo la Serikali Namba 255 la mwaka 2017.

Aidha, kwa kushirikiana na wataalamu wa Misitu kautoka Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu(TSF) Wilaya ya Iringa na Kikosi cha Ujangili (KDU) tulifanikiwa kuokoa mazao ya misitu ikiwa ni magogo 52, mitumbwi 32 na mizinga 12 kutokana na uvunaji haramu uliofanyika katika msitu huo.

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Majukumu ya TAKUKURU kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 Kifungu cha 7 ni kuchunguza na kushtaki watuhumiwa, kutoa Elimu ya Rushwa kwa jamii (Umma) , kutoa ushauri kwa Serikali , Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi kuhusu namna bora ya kuzuia Rushwa na kufanya Utafiti wa Mifumo inayoweza kusababisha Rushwa.

Kwa kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Iringa imeweza kutekeleza majukumu hayo kama ifuatavyo:-

1. **UCHUNGUZI**

Katika kipindi cha April hadi Juni, 2020 TAKUKURU (M) Iringa ilipokea malalamiko **68** ambapo baadhi ya walalamikaji walishauriwa na taarifa nyingine zilihamishiwa Idara zingine, na zile zinazohusu Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 ziko kwenye hatua mbalimbali za uchunguzi ambapo mashtaka **16** yamefikishwa Mahakamani katika kipindi husika .

2. **ELIMU KWA UMMA**

Katika kipindi husika, uelimishaji umma kuhusu madhara ya vitendo vya rushwa ulifanyika , katika uelimishaji huo jumla ya semina **21** zilitolewa kwa wadau mbalimbali, zimeimarishwa klabu za wapinga rushwa **18** mikutano ya hadhara 0**7** imefanyika**,** zimetayarishwa makala na habari **06,** vipindi vya redio **04** vilifanyika na taarifa **07** kwa Vyombo vya habari zilitolewa**.** Kupitia Elimu kwa Umma Jumla ya wananchi 931 walifikiwa.

3. UTAFITI NA UDHIBITI

Ndugu wanahabari,

Katika kipindi husika , kazi za utafiti na udhibiti zilizofanyika ni pamoja na uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (public expenditure tracking survey-pets).

UCHAMBUZI WA MIFUMO NA UDHIBITI

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa ilifanya uitekelezaji wa kazi za uchambuzi wa mifumo na udhibiti kama ifuatavyo:-

1. Uchambuzi wa mfumo wa upangaji madaraja ya ununuzi wa nishati ya umeme ofisi ya TANESCO (W) Mufindi ambapo baadhi ya wateja walikuwa wamewekwa kwenye madaraja wasiyostahili ya ununuzi wa umeme. Aidha, uchambuzi na ufuatiliaji maazimio ya utekelezaji umekamilika na wateja 11 wa eneo la Mgololo wamerejeshwa katika daraja stahili.
2. Uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa njia ya kielekroniki kwa kutumia mashine za POS (Point of Sale) katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga.
3. Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji vyama vya Ushirika wa mazao (AMCOS) katika Halmashauri za Manispaa ya Iringa, Halmashauri za Wilaya ya Iringa, Mufindi na Kilolo.
4. Uchambuzi wa mfumo katika usimamizi na udhibiti wa hifadhi asili ya Kilombero Wilayani Kilolo.
5. Udhibiti wa malipo ya posho ya safari kwa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwenda Dodoma, safari ambayo haikufanyika ambapo kiasi cha **shilingi 4,243,200/=** ziliokolewa.

6. Udhibiti wa mazao ya misitu (magogo 52, mitumbwi 32 na mizinga 12) katika hifadhi ya mlima Idelema kijiji cha Makifu Tarafa ya Idodi Wilaya ya Iringa ambapo kiasi cha **shilingi 20,572,434.00** zilidhibitiwa.
7. Uchambuzi wa mfumo wa ukadiriaji wa kodi ya PAYE na SDL katika Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Iringa ambapo ukwepaji wa malipo ya kodi hizo uliokuwa unafanywa na Uongozi wa Kiwanda cha Hongwei International Co.Ltd cha Mafinga ulifanyiwa udhibiti na kiasi cha **shilingi. 198,719,497. 17** ziliokolewa.

- **UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA UMMA (PUBLIC EXPENDITURE TRACKING SURVEY-PETS)**

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa ilifuatilia jumla ya miradi minane (8) katika sekta za Afya, Elimu , Ujenzi, Maliasili (Misitu) na Utawala yenye thamani ya jumla ya shilingi **Bilioni moja milioni mia tatu ishirini mia sita sitini na nne mia mbili themanini na moja na senti thelathini na tano** (**1,320,664,281/35**) kwa lengo la kujua endapo rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo zimewafikia walengwa kwa wakati na kuangalia kama kiasi cha fedha kilichotumika kinalingana na ubora wa kazi au huduma inayotolewa kwa walengwa (thamani ya fedha) kama ifuatavyo:-

1. Mradi wa ulinzi na usalama wa mtoto (UNICEF) katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa wenye thamani ya **shilingi 755,664,281.35 .**
2. Mradi wa ujenzi wa jengo la Uchunguzi katika Hospitali ya FRELIMO katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wenye thamani ya **shilingi 400,000,000/=.**
3. Mradi wa ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika shule ya sekondari IGUMBILO katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wenye thamani ya **shilingi 45,000,000/=.**

4. Mradi wa ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika shule ya sekondari MAKIFU katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa wenye thamani ya **shilingi 120,000,000/=** .
5. Mradi wa ukamilishaji wa ujenzi wa soko la Luganga katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo wenye thamani ya **shilingi 265,000,000/=.**
6. Mradi wa ukarabati wa madarasa mawili (2) yaliyoezuliwa na upepo shule ya sekondari Igombavanu katika Halmashauri ya wilaya ya Mufindi wenye thamani ya **shilingi 17,622,000/=.**
7. Ufuatiliaji wa fedha **shilingi 350,000,000/=** za wavunaji msitu SAO HILL (UWASA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.
8. Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha **shilingi 26,000,000/=** za mfuko wa jimbo katika Halmashauri ya mji Mafinga.

Aidha, katika ufuatiliaji huo miradi minne (4) ambayo ni; Mradi wa ulinzi na usalama wa mtoto (UNICEF), Mradi wa ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika shule ya sekondari MAKIFU, Ufuatiliaji wa fedha **shilingi. 350,000,000/=** za wavunaji msitu SAO HILL (UWASA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi , Mradi wa ukarabati wa madarasa mawili (2) yaliyoezuliwa na upepo shule ya sekondari Igombavanu ilibainika kuwa na kasoro .

Miradi ~~miradi~~ miwili ambayo ni ulinzi na usalama wa mtoto (UNICEF) katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na Mradi wa ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika shule ya sekondari MAKIFU inachunguzwa ambapo Mradi wa Ufuatiliaji wa fedha za wavunaji msitu SAO HILL (UWASA unafanyiwa udhibiti na Mradi wa ukarabati wa madarasa mawili (2) yaliyoezuliwa na upepo shule ya sekondari Igombavanu ulitolewa mapendekezo ya kufanyiwa marekebisho .

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU (M) Iringa imejipanga kuendelea na majukumu yake katika robo ya mwaka mpya wa fedha **Julai hadi Septemba, 2020** ambapo kipaumbele kimewekwa katika suala zima la uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Pia tutaendelea na operesheni za urejeshwaji wa fedha kutoka kwa wadaiwa sugu wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) , Vyama vya Ushirika vya Mazao na Biashara (AMCOS) na Vyama Vikuu vya Ushirika , ikiwa ni pamoja na kuendelea na chunguzi za ubadhirifu wa fedha za Vyama vya Ushirika .

"Kupambana na rushwa ni jukumu langu"

Imetolewa na:

SGN
Mweli Evart Kilimali,
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA IRINGA